



Wanachama wa FoodShare:


Unaweza kupata manufaa zaidi ya FoodShare ikiwa una gharama za matibabu unazolipia kwa pesa zako mwenyewe.

(FoodShare Members: You may be able to get more FoodShare benefits if you have medical expenses that you pay out of your own pocket.)

- Je, unapata manufaa ya FoodShare?
- Je, una umri wa miaka 60 au zaidi, kipofu, au wewe ni mlemavu?
- Je, una gharama za matibabu unazolipia kwa pesa zako mwenyewe?

Ikiwa umejibu "Ndiyo" kwa maswali yote matatu, unaweza kupata manufaa zaidi ya FoodShare. Hii ni kwa sababu unaweza kupata muamana kwa baadhi ya pesa unazotumia kwenye gharama fulani za matibabu. Hii inaitwa kupata makato ya gharama za matibabu.

Mifano ya gharama za matibabu zinazostahiki ni pamoja na:



Dawa za agizo la daktari



Dawa za kununua bila agizo la daktari



Malipo ya bima



Miwani na lenzi za kuambatanisha na mboni

Pata maelezo zaidi:

Ili kupata maelezo zaidi kuhusu jinsi ya kupata manufaa zaidi ya FoodShare kwa kuripoti baadhi ya gharama za matibabu, wasiliana na wakala wa eneo lako kwa simu, barua, faksi, au ana kwa ana.

Unaweza kupata wakala wa eneo lako kwa kutembelea dhs.wi.gov/forwardhealth/imagency/index.htm.

Kwa habari zaidi kuhusu kazi ya makato ya gharama za matibabu, angalia mwongozo kamili mtandaoni kwenye: www.dhs.wisconsin.gov/publications/p03315b.pdf.

Bado hujaanza kupata manufaa ya FoodShare? Kuna njia nne za kutuma ombi:

Mtandaoni. Tuma ombi kwenye tovuti ya ACCESS katika access.wi.gov.

Kwa simu. Ili kutuma ombi kwa simu, piga simu kwa wakala wa eneo lako.

Kwa barua au faksi. Ili kutuma ombi kwa barua au faksi, tuma ombi lililojazwa kwa wakala wa eneo lako.

Ana kwa ana. Ili kutuma ombi ana kwa ana, tembelea wakala wa eneo lako. Huenda ukahitaji kuweka miadi.

Mradi huu umefadhiliwa angalau kwa sehemu na fedha za Serikali Kuu kutoka kwa U.S. Department of Agriculture (Wizara ya Kilimo ya Marekani). Mambo yaliyo kwenye chapisho hili si lazima yaonyeshe mtazamo na sera za U.S. Department of Agriculture (Wizara ya Kilimo ya Marekani), wala kutajwa kwa majina ya biashara, bidhaa za biashara, au mashirika hakumaanishi kwamba Serikali ya Marekani inaunga mkono.